

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

621


KISWAHILI

Muda: Saa 3


Jumanne, 08 Mei 2018 mchana

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C yenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)**, sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Ukurasa wa 1 kat i ya 3



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Bainisha mambo manne ya kuzingatia ili kuwepo mawasiliano kati ya mzungumzaji na msikilizaji.
2. Eleza kwa kifupi sifa nne za vitendawili.
3. Fafanua kwa kifupi mambo manne ya kuzingatia katika utungaji wa mazungumzo.
4. Orodhesha mbinu nne utakazotumia kufundishia usupisho katika somo la Kiswahili.
5. Chambua kwa kifupi faida nne za fasihi simulizi katika jamii.
6. Taja vifaa vinne vya mtaala wa somo la Kiswahili shule za msingi.
7. Ainisha sifa nne za shairi la kimapokeo.
8. Bainisha aina nne za vielezi, kisha tunga sentensi moja kwa kila aina.
9. Orodhesha aina nne za maswali ya ufahamu, kisha toa mfano kwa kila aina.
10. Eleza kwa kifupi mambo manne muhimu ya kuzingatia unapotumia mbinu ya ziara kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili** (2) kutoka katika sehemu hii.

11. Eleza mambo matano ya kuzingatia unaposanya usupisho wa habari.
12. Fafanua sehemu nne za utungaji wa risala.
13. Bainisha manufaa matano ya vitendawili katika jamii.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii.

14. Bainisha faida tano za upimaji wa wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
15. Chambua mambo matano utakayozingatia wakati wa kutayarisha zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.
16. Fafanua manufaa matano ya muhtasari kwa mwalimu wa somo la Kiswahili.